



CHUO KIKUU MZUMBE

KUAHIRISHA UDAHILI WA WANACHUO KATIKA KITUO CHA KUFUNDISHIA CHA MWANZA KATIKA MWAKA WA MASOMO 2017/2018

Chuo Kikuu Mzumbe kimeahirisha udahili wa wanachuo wa programu zote zinazotolewa katika Kituo cha Kufundishia cha Mwanza cha Chuo Kikuu Mzumbe kwa mwaka wa masomo 2017/2018 kufuatia maagizo ya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Baada ya uhakiki uliofanywa na TCU kwa vyuo vikuu vyote nchini mwezi Oktoba mwaka 2016, TCU imekiagiza Chuo Kikuu Mzumbe kusitisha udahili wa wanachuo wapya katika Kituo hiki mpaka Chuo Kikuu Mzumbe kitakapokamilisha masharti yaliyowekwa na TCU kwa ajili ya Vituo vya Kufundishia yatakapokamilishwa. Tayari menejimenti ya Chuo Kikuu Mzumbe imeanza kuyafanyiakazi maagizo ya TCU kwani kisheria ndio mamlaka ya usimamizi wa vyuo vikuu hapa nchini. Hata hivyo, maagizo haya hayawahusu wanachuo wanaoendelea na masomo au waliohitimu programu mbalimbali katika Kituo hiki.

Aidha Chuo Kikuu Mzumbe kinaendelea na mpango wake wa muda mrefu wa kusogeza huduma zake za kutoa taaluma, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu, Kanda ya Ziwa kwa kununua eneo la ekari takribani 220 katika Kijiji cha Kabusungu, Kata ya Sangabuye, katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela katika Mkoa wa Mwanza. Mchakato wa ununuzi wa eneo hili unaendelea.

Karibuni, *Tujifunze Kwa Maendeleo Ya Watu!*

Rainfrida Ngatunga
Mkurugenzi wa Mawasiliano
Chuo Kikuu Mzumbe
S. L. P 1, Mzumbe
Email: dc@mzumbe.ac.tz